SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA
(MAMLAKA ZA WILAYA) NO.7 YA 1982

SURA 287
ZIMETUNGWA CHINI YA KIFUNGU NA 153
SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIMANJIRO 2016

1. **SURA YA KWANZA**

UTANGULIZI

Katika kipengele cha tafsiri yaongezwe maneno yafuatayo:-

"Seremala"maana yake fundi wa thamani za mbao au fundi yeyote anayejishugulisha na kazi za kutengeneza thamani za mbao.

"Fundi uashi" maana yake ni kikundi/mtu ambaye anajishughulisha na ujenzi wa majengo lakini hajajisajili na Bodi ya wakandarasi Tanzania.

"Magari Binafsi" maana yake ni magari yanayoendeshwa na wamiliki au wasio wamiliki kwa shughuli binafsi.

"Mabango /Matangazo" Maana yake ni nembo /alama yoyote ama ya kuchora inayoonyesha/ashiria/tambulisha shughuli za biashara za kampuni/taasisi /mtu binafsi na hii ni pamoja na maandishi yaliandikwa ukutani, kibao/ ubao, sehemu yoyote.

"Madini "maana yake ni pamoja na miamba aina zote, mawe,mchanga au madini yote yanayotambuliwa chini ya sheria ya madini namba 14 za mwaka 2010 pamoja na Marekebisho yake;

"Ushuru wa kuegesha magari katika vituo mbalimbali "maana yake ni ushuru ambao gari/pikipiki/pikipiki za magurudumu matatu yoyote itakayoegeshwa katika eneo la Halmashauri itapaswa kulipwa lakini haitajumuisha maeneo binafsi.

"Mabasi Makubwa" maana yake ni mabasi yanayochukua kuanzia abiria 30 hadi 60.

"Mabasi madogo" Maana yake ni mabasi yanayochukua abiria chini ya 30.

"Lori" Maana yake ni Magari makubwa ya mzigo kuanzia tani tatu na kuendelea yaliyotengenezwa na kuruhusiwa na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kubeba mizigo.

"Magari madogo ya mizigo" Maana yake ni magari madogo ya mizigo chini ya tani tatu yaliyotengenezwa na kuruhusiwa na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kubeba mizigo.

2. Sheria ndogo za ada na ushuru za Halmashauri za Mwaka 2010 kama ifuatavyo:-

A: Ushuru wa kuegesha gari katika kituo cha mabasi na teksi isomeke "ushuru wa kulaza/ kuegesha magari katika vituo vya mabasi/stendi na teksi, au eneo lolote lile lililoruhusiwa na Halmashauri.

ADA NA USHURU.

(i) Mabasi makubwa kutoka TShs 2,000/= hadi Tshs. 3,500/ kwa siku
(ii) Mabasi madogo (mini buses) kutoka Tshs. 1,000/= hadi Tshs. 2,500/kwa siku
(iii) Magari madogo ya abiria (Teksi,Landrover) kutoka Tshs,500/= hadi Tshs 1,500/- kwa siku
(iv) Magari madogo ya mizigo kutoka Tshs. 1,000/= hadi Tshs. 2,500/= kwa siku
(v) Pikipiki ya magurudumu matatu ya kubebea abiria kutoka Tshs. 300/= hadi Tshs, 500/= kwa siku.

BAADA YA HAPO VIONGEZWE VIPENGELE VIFUATAVYO:-

(i) Pikipiki (Bodaboda) iwe Tshs 200/= kwa siku
(ii) Pikipiki ya magurudumu matatu ya mizigo iwe Tsh. 1,000/= kwa siku

BAADA YA HAPO IONGEZWE:-

A(1) Ushuru wa kuegesha gari/magari katika vituo mbalimbali katika eneo lolote lililotengwa kwa ajili ya kuegesha gari/magari ndani ya eneo lote la Mamlaka la Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro

i. Mabasi makubwa Tshs 3,500/= kwa siku
ii. Mabasi madogo (Mini Buses) Tshs 2,500/= kwa siku
iii. Magari madogo ya mizigo (pickup) Tshs 2,500 kwa siku
iv. Magari madogo ya abiria (Teksi/Cab/Landrover) Tshs 5,000/= kwa siku
v. Lori Tshs. 3,500/= kwa siku
vi. Pikipiki ya magurudumu matatu ya kubeba abiria Tshs. 500/= kwa siku
vii. Pikipiki Tshs 200/= kwa siku
viii. Pikipiki magurudumu matatu ya mizigo (Toyo) Tshs 1,000/=kwa siku
ix. Magari binafsi ya kutembelea Tshs. 500/= kwa siku.

B: USHURU WA VYOMBO VYA MOTO VYOTE VINAVYOTOKA STENDI.

i. Mabasi makubwa kutoka Tshs 1,000/=@ linapotoka hadi 2,000/=
ii. Mabasi madogo kutoka 500/= @ linapotoka hadi Tshs 1,000/=
iii. Lori kutoka Tshs. 1,000/= @ linapotoka hadi Tshs. 2,000/=

iv. Magari madogo (mini Buses) kutoka Tshs. 500/= @ linapotoka hadi Tshs 1,000/=
v. Magari madogo ya mizigo kutoka Tshs 500/= @ linapotoka hadi Tshs. 1,000/=

Ipunguzwe kutoka Tshs.300/= hadi Tshs. 200/=@ linapotoka stendi.

BAADA YA HAPO VIONGEZWE VIPENGELE VIFUATAVYO;-

(i) Pikipiki ya biashara Tshs. 200/= @ inapotoka stendi
(ii) Pikipiki isiyokuwa ya biashara Tshs. 200/= @ inapotoka stendi
(iii) Magari binafsi yasiyo ya biashara Tshs.1,000/= @ inapotoka stendi
(iv) Pikipiki ya magurudumu matatu ya mizigo (Toyo) Tshs. 500/= inapotoka stendi
(v) Huduma ya choo cha stendi Tshs. 300/=@ mtumiaji anayetumia.

JEDWALI LA PILI

ADA YA VIBAO VYA MATANGAZO YA BIASHARA YALIYOSIMIKWA, KUCHORWA, KUCHAPISHWA, KUBANDIKWA KATIKA ENEO.

Jedwali la pili la sheria ya ada na ushuru linalohusu ada na matangazo linarekebishwa kwa kubadilisha viwango vya fedha za ushuru na matangazo kama ifuatavyo;-

(i)	Maombi ya kufanya matangazo…….	Sh. 5,000/=
(ii)	Yasiyowaka taa (non-illuminated)…….	Sh. 20 kwa sentimeta moja za mraba kwa mwaka.
(iii)	Lenye mwanga (illuminated Advertisement...	Sh. 25 kwa Sentimeta moja za Mraba kwa mwaka.
(iv)	Meza na viti vilivyowekwa matangazo…….	Kila kimoja Sh. 10 kwa kila sentimeta moja za mraba.
(iv)	Matangazo mengine yoyote …….	Sh. 15 kwa Sentimeta.

JEDWALI LA TATU
USHURU WA MACHINJIO NA UKAGUZI WA NYAMA
A: USHURU WA KUKAGUA NYAMA

(i) Ng'ombe kutoka Tshs 1,000/= hadi shs. 2,000/= @ kichwa
(ii) Mbuzi/Kondoo kutoka Tshs.500/= hadi Tshs 1,000/= @ kichwa
(iii) Wanyama wengine kutoka Tshs. 500/= hadi Tshs 1,000/= @ kichwa.

B: USHURU WA KUTUMIA MACHINJIO

i. Ng'ombe kutoka Tshs. 3,000/= hadi Tshs. 5,000/=@ kichwa.
ii. Mbuzi/Kondoo kutoka Tshs 1,000/= hadi Tshs 3,000/= @ kichwa

C: USHURU WA KUKUSANYA NGOZI

Aina ya ngozi.

(1) Ngozi ya ng'ombe kutoka Tshs 500/= hadi Tshs. 1,500/= @ ngozi
(2) Ngozi ya mbuzi/ kondoo kutoka Tshs 200/= hadi Tshs.500/= @ ngozi.

JEDWALI LA NNE
KATIKA JEDWALI HILI ISOMEKE USHURU WA VIBANDA /VYUMBA VYA SOKO, MEZA (KIZIMBA) BADALA YA USHURU WA VIBANDA.

1. Kibanda kutoka Tshs. 10,000/= @ mwezi hadi Tshs 30,000/= @ mwezi
2. Meza/ Kizimba Tshs. 200/= kwa siku kwa mwezi Tsh 6000/=

PIA KATIKA HILI, IONGEZWE SEHEMU "B" USHURU WA SEREMALA NA UFUNDI WASHI.

1. SEREMALA THS. 500/= @ SIKU
2. FUNDI UASHI TSHS. 50,000/= @ UJENZI ANAOUFANYA

SEHEMU (B)
ADA ZA KUKODI MAGARI NA MITAMBO YA HALMASHAURI

(a) Ada ya kukodi magari ya Halmashauri

i. Lori tani 3 hadi 7 kutoka Tshs 100,000/= @ siku hadi 150,000/= siku
ii. Lori tani 7 na zaidi toka Tshs. 130,000/= @ siku hadi Tshs 200,000/= @ siku.
iii. Magari madogo kutoka Tshs 1,000/= @ kilometa hadi Tshs 2,000/= @ kilomeita
iv. Mkataba unaweza kutoa bei tofauti kwa makubaliano ya pande mbili,na itakuwa bei halali inayotambulika na sheria ndogo hii.

B: Ada ya kukodi mitambo

1. Bull dozer D6C. kutoka Tshs. 380,000/= @ siku hadi Tshs 500,000/= @ kwa masaa nane ya siku.
2. Back hoe 428D kutoka Tshs. 320,000/= hadi Ths. 480,000/= kwa masaa nane ya siku kwa wakandarasi wote.
3. Back hoe 428D kutoka Tshs. 160,000/= @ siku hadi Tshs.240, 000/= kwa masaa nane ya siku au Tshs. 50,000/= kwa kila saa lakini ni kwa wananchi wa kawaida wa Simanjiro na ambao si wakandarasi.
4. Na mitambo mingine itakayofanana au ya aina ya bull dozer na back hoe itakodishwa kwa Tsh 500,000/= kwa masaa nane ya siku.

5. Gharama ya mafuta na vilainishi katika ukodishaji wa magari na mitambo itakuwa ni juu ya mkodishaji.
6. Magari na mitambo hiyo itaendeshwa na madereva wa Halmashauri ambapo mkodishaji atagharamikia posho za madereva/dereva.

SEHEMU E

(iv) USHURU WA MIFUGO ILIYOINGIA MNADANI

1. Ng'ombe, Pumba , Farasi, Ngamia na wengine kama hao Tsh 2000/= kwa kichwa cha mfugo.
2. Mbuzi, Kondoo, Tsh 1000/= kwa kichwa cha mfugo.
3. Wanyama wengine wafugwao Tsh. 1000/=

(v) USHURU WA MIFUGO ILIYOUZWA MNADANI NA KUTOKA

1. Ng'ombe, Punda,Farasi, Ngamia na wengine kama hao Tsh. 5000/=
2. Mbuzi, Kondoo, na wengine kama hao Tsh. 1000/= kwa kichwa cha mfugo.
3. Wanyama wengine wafugwao Tsh 1000/= kwa kila kichwa cha mfugo.

SEHEMU (F)
USHURU WA NJIA ZA MIFUGO

1. Ng'ombe/Punda na wengine kama hao kutoka Tshs. 1,000/= hadi Tshs. 1,500/= @ kichwa
2. Mbuzi/ Kondoo/na wengine iwe Tshs. 500/= @ kichwa

SEHEMU "G" MAJINA YA MINADA/SOKO YAONGEZWA MANENO YAFUATAYO:-

KATA YA LOIBORSIRET

18. **NARAKAUO** na

Sheria ndogo hii itatambua maeneo mengine yote yatakayoibuliwa kuwa Masoko/Soko na Mnada kupitia vikao vya Halmashauri ya Wilaya ya Simanjiro kuwa ni vyanzo halali vya mapato tangu kupitishwa sheria hii na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

JEDWALI (A)

USHURU WA MADINI YA UJENZI

AINA YA MADINI	**KIASI CHA USHURU**
1. Mchanga ……..Kwa kila 1M^3	Tsh. 3,500/=
2. Mawe ……kwa kila 1M^3	Tsh 3,500/=
3. Kokoto …….kwa kila 1M^3	Tsh 3,500/=
4. Changarawe/ Moramu …….Kwa kila 1M^3	Tsh 3,500/=

JEDWALI "B" LA USHURU WA MADINI YA UJENZI

Kiongezwe chanzo cha LERUMO na sehemu nyingine itakayoibuliwa na Kuitambua na Halmashauri kuwa chanzo cha madini ya mchanga.

JEDWALI LA KWANZA.
USHURU WA SAMAKI, VIWANGO VYA USHURU VIBADILIKE NA KUSOMEKA

(1) Samaki Kavu
  (a) Tenga kubwa Tsh 15,000/=
  (b) Tenga Kati Tsh 7,500/=
  (c) Tenga Dogo Tsh 3,500/=
(2) Samaki mbichi @ Pickup Tsh 70,000/=

KATIKA JEDWALI HILI LA PILI SEHEMU YA "H" LA USHURU HUU YAONGEZEKE MAJINA YAFUATAYO:-

KITUO	**MAHALI**
Kidawashi	Kata ya Shambarai

KODI YA HUDUMA
MAREKEBISHO YAFANYIKE KATIKA MAENEO YA TAFSIRI NA UTOZAJI WA USHURU.

TAFSIRI
Badala ya Taasisi ya Kibiashara isomeke "Mfanyabiashara" maana yake Mtu yeyote,Kampuni, Mbia aliyesajiliwa na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufanya biashara na ana leseni iliyotolewa na Mamlaka husika ya utoaji wa leseni kwa ajili ya biashara anayofanya, kwa mujibu wa sheria ya leseni za Biashara namba 25 ya 1972 (R.E 2002) pamoja na marekebisho yake.

UTOAJI USHURU

HALMASHAURI ITATOZA NA KUKUSANYA USHURU WA HUDUMA KWA MUJIBU WA SHERIA NDOGO HIZI KILA MFANYABIASHAA SIO TAASISI YA KIBIASHARA.
Pia katika utozaji wa ushuru huu yaongezwe mananeo kuwa "ushuru utatozwa hadi kwenye maeneo ambako biashara inafanyika au katika matawi ya biashara na siyo tu kwenye makao makuu ya biashara au ya uzalishaji

MENGINEYO

Sheria ndogo hizi zinatambua maelekezo yote ya Serikali Kuu yaliyotolewa kabla na yatakayotolewa baada ya Sheria ndogo hizi kuanza kutumika ya namna ya Ukusanyaji wa Ushuru wa Halmashauri na Vijiji na Kupitia kikao cha Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango cha Tarehe 25/11/2016 ambapo kikao kiliadhimia ili vijiji vyote viweze kuwa na maendeleo kwa kupata huduma za msingi na lazima, kama Maji, Afya, Elimu na huduma nyingine za kufanana na hizo ni lazima Halmashauri kuongeza usimamizi wa fedha kwa vijiji vyenye fursa zaidi ya vyanzo vya mapato, na katika mapato ya vijiji hivyo asilimia 60% itakuwa ni mapato ya Halmashauri kusaidia uendeshaji wa shughuli mbalimbali za Halmashauri na asilimia 40% itabaki katika Kijiji husika kuendeleza miradi ya Maendeleo.

ADHABU.

Adhabu mbadala faini isiyozidi Tshs. 50,000/= isomeke adhabu isiyopungua Tshs. 50,000/= na isiyozidi Tshs.300,000/= au kifungo cha miezi kumi na mbili jela au adhabu zote mbili kwa pamoja(kifungo na faini.) Aidha, faini iliyotozwa haita athiri kwa Halmashauri kurejeshewa fedha zilizotumika katika kuzuia ukiukwaji au kwa ukiukwaji uliofanywa wa sheria ndogo hizi.

Nembo na mhuri wa Halmashauri ulibandikwa kwenye sheria ndogo hizi kufuatana na azimio hili lililopitishwa kwenye mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe ……..mwezi ……mwaka……na kuthibitishwa:-

……..

YEFRED MYENZI
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
SIMANJIRO

……
JASCKSON LESIKAR SIPITIECK
MWENYEKITI WA HALMASHAURI
HALMASHAURI YA WILAYA
SIMANJIRO

NIMEKUBALI

DODOMA
TAREHE……..... **…….**
RAIS GEORGE B. SIMBACHAWENE (MB)
WAZIRI WA NCHI- OR-TAMISEMI